



**Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika  
(WILDAF)**

# **ATHARI ZA KIAFYA ZA UKATILI MAJUMBANI**

## **Haja ya Kuwa na Sheria Dhidi ya Ukatili Majumbani**

**Muhtasari wa Sera**

**Suala la: 4**

**Septemba, 2021**





**WILDAF**

**Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika  
(WILDAF)**

## **ATHARI ZA KIAFYA ZA UKATILI MAJUMBANI**

### **Haja ya kuwa na Sheria dhidi ya Ukatili Majumbani**

**Muhtasari wa Sera**

**Suala la: 4**

**Septemba, 2021**



## UTANGULIZI

Ukatili majumbani ni aina ya ukatili unaofanywa na mtu katika mazingira ya wanafamilia wanaoishi katika nyumba moja. Ukatili majumbani pia unajumuisha ukatili wa kimwili, ukatili wa kingono, vitisho, ukatili wa kiuchumi, na ukatili wa kihisia / kisaikolojia. Ukatili majumbani hauishii tu kwa wanandoa na Watoto, bali huenda zaidi kwa watu wanaishi Pamoja kama wapenzi, mashemeji, wafanyakazi wa ndani na ndugu wengine wanaoishi katika familia moja.

Wanawake na watoto ambao wanakumbana na ukatili majumbani wako katika hatari ya kupata athari za kiafya ikiwemo majeraha, magonjwa kama vile HIV/ AIDs pamoja na magonjwa mengine ya ngono, ukosefu wa huduma za afya, ukosefu wa chakula chenye lishe nk. Vile vile wanawake na watoto wako katika hatari ya kupata athari za kisaikolojia kama msongo wa mawazo pamoja na magonjwa mengine.

Muhtasari huu wa sera unaainisha athari za kiafya zinazotokana na ukatili majumbani. Pia muhtasari unatoa mapendekezo kwa watunga sera kuona haja ya kutunga sheria dhidi ya ukatili majumbani ili kupunguza athari za kiafya zinazoambatana na ukatili majumbani dhidi ya wanawake na watoto.



## KUENEA KWA UKATILI MAJUMBANI TANZANIA

- Kwa mujibu wa ripoti ya Benki ya Dunia (2008), wanawake wanaoishi vijijini nchini Tanzania wako katika hatari kubwa ya ukatili majumbani, kwa kuwa mifumo ya ulinzi dhidi ya wanawake haifahamiki kwa wanawake wengi walioko vijijini.
- Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya Tanzania (TDHS 2015/16) ulibaini kuwa wanawake wanne kati ya kumi wamefanyiwa ukatili wa kimwili au kingono katika maisha yao.
- Kwa mujibu wa ripoti ya Umoja wa Mataifa ya Wanawake, Ukatili wa Kingono, Kimwili, na Kisaikolojia hutokea sana kwa wanawake walioolewa nchini Tanzania (UN Women 2019).
- Ripoti ya TDHS ilibaini kuwa asilimia 58 ya wanawake wanaamini kwamba kupigwa kwa mke kunakubalika ikilinganishwa na asilimia 40 ya wanaume wanao amini hivyo.
- Utafiti wa Shirika la Afya Duniani (WHO) uliofanywa jijini Dar es Salaam na Mbeya mwaka 2005 ulibaini kuwa asilimia 60 ya wahanga wa ukatili majumbani hawajawahi kuomba msaada kwa sababu waliamini kuwa ukatili uliofanywa na wenza wao ulikuwa 'wa kawaida' hivyo hawakutafuta msaada.

### Mifumo ya Kisheria na Mahakama

Serikali ya Tanzania imerekebisha na kupitisha sheria kadhaa za kuimarisha haki za wanawake, ikiwa ni pamoja na Sheria ya Makosa ya Kujamiiana, ya mwaka 1998 (SOSPA), ambayo inalinda wanawake na watoto dhidi ya unyanyasaji wa kingono. Hata hivyo, SOSPA haijaongelea kuhusu ubakaji wa kwenye ndoa wala ukatili majumbani.

Sheria ya Ndoa namba 29 ya mwaka 1971, inakataza adhabu dhidi ya mke au mume lakini sheria hii haijatoa adhabu dhidi ya wahalifu wa ukatili huo. Mwaka 2016/17, Serikali ilipitisha Mpango kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), kutokomeza ukatili na kuhakikisha upatikanaji wa haki. Vile vile mpango kazi huu unalenga kuimarisha huduma za upatikanaji wa huduma kwa wahanga ikiwemo kuanzisha vituo vya mkono kwa mkono (One stop Centres) ili kuhakikisha wahanga wanapata huduma za afya, sheria, ushauri wa kisaikolojia na huduma nyingine katika kituo kimoja. Hata hivyo mpaka kufikia mwaka 2019 serikali imefanikiwa kuanzisha vituo 13 tu nchi nzima. Utekelezaji wa MTAKUWWA unakwenda taratibu kutokana na ukosefu



wa sheria kama sheria dhidi ya ukatili majumbani ili kurahisisha utekelezaji wa mpango kazi.

Sheria zinazosimamia haki kwa wahanga wa ukatili majumbani hazitoi kinga na ulinzi wakutosha kwa wanawake wanaoopeleka kesi zao mahakamani. Kwa mfano nchi za jirani kama Kenya na Africa Kusini katika sheria zao dhidi ya ukatili majumbani mhanga wa ukatili anaweza kuomba amri ya mahakama kumuondoa mhalifu pale nyumbani mpaka kesi itakapokamilika na kutolewa maamuzi. Hata hivyo, kutumika kwa sheria za kimila na kidini zinapunguza uwezekano wa wahanga wa ukatili majumbani kupata haki.

Mwaka 2017 Serikali ilipitisha Sheria ya Msaada wa Kisheria Na.1 ya mwaka 2017. Lengo ni kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa watu wasiojiweza, kutambua wasaidizi wa kisheria kama moja ya mikakati ya kuhakikisha haki inapatikana kwa wanawake na watoto walioathirika na ukatili. Hata hivyo sheria hii inalenga zaidi kushughulikia kesi ambazo tayari zimeshatokea na sio kuzuia ukatili wa kijinsia hasa majumbani.




## ATHARI ZA KIAFYA ZA UKATILI MAJUMBANI

Pamoja na jitihada za Serikali, ukatili majumbani bado upo na unaendelea kuongezeka nchini Tanzania. Aina hii ya ukatili ni mbaya zaidi kwa kuwa inafanyika nyumbani sehemu ambayo ingetegemewa kuwa salama. Ripoti zinaonyesha kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya ukatili majumbani na athari za kiafya. Baadhi ya athari za kiafya ni pamoja na maambukizi ya VVU, maambukizi ya magonjwa ya zinaa (STDs). Zaidi ya hayo, ukatili majumbani unaweza kusababisha utoaji mimba wa kulazimishwa, kuzaliwa watoto wenye uzito mdogo, watoto kuzaliwa mapema kabla ya muda, kuongezeka kwa tabia hatarishi za kiafya kama matumizi ya pombe, kujiua, majeraha ya mwili, na vifo kwa wahanga wa ukatili. Yafuatayo ni madhara ya kiafya yatokanayo na ukatili majumbani;


### a) Maambukizi ya VVU na magonjwa mengine ya zinaa (STD)

Kuna ushahidi kwamba ukatili majumbani, hasa ukatili dhidi ya wenza (IPV), unahatarisha afya ya wanawake na wasichana. Wanawake na wasichana wengi huambukizwa VVU na magonjwa ya zinaa kutokana na kukosa maamuzi juu ya afya zao lakini pia kutokana na kufanya ngono ya kulazimishwa. Wanawake wanaopitia ukatili au wanaoishi kwa hofu ya kufanyiwa ukatili wanaweza kuwa na maamuzi kidogo juu ya muda au utayari wao kufanya ngono au uwezo wa kujadili matumizi ya kinga. Kwa mujibu wa ripoti ya TACAIDS (2020) ilibaini kuwa;

- Wanawake na wasichana wanaendelea kubeba mzigo wa maambukizi VVU nchini Tanzania. Ambapo, mwaka 2018 kulikuwa na watu 1,600,000 wanaoishi na VVU nchini Tanzania. Kati yaowenye umri wa miaka 15 na zaidi, kulikuwa na wanawake 880,000 wanaoishi na VVU ikilinganishwa na wanaume 580,000 wanaoishi na VVU.



- Vile Vile report ya mwaka 2018, ilibainisha kwamba wasichana balehe na wanawake wadogo 54,000 wenye umri wa miaka 10-19 walikuwa wakiishi na VVU, ikilinganishwa na wavulana 39,000 wa umri huo. (UNAIDS taarifa, 2019)



Source: GENDER ASSESSMENT OF THE NATIONAL HIV/AIDS RESPONSE - ADVOCACY BRIEF TANZANIA (MAINLAND) 2020

- Ndani ya mwaka 2018, kulikuwa na maambukizi mapya ya VVU 36,000 kwa wanawake na 27,000 kwa wanaume wenye umri wa miaka 15-49
- Miongoni mwa vijana wenye umri wa miaka 15-19, idadi ya maambukizi mapya miongoni mwa wasichana ni karibu mara tatu zaidi kuliko ile ya wavulana
- Kuna maambukizi mapya 8002 kila mwaka kwa wasichana wadogo wa umri wa miaka 15-19, zaidi ya mara mbili ya idadi ya maambukizi mapya miongoni mwa wavulana (2876).
- Miongoni mwa wasichana, kuna maambukizi mapya 7986 kila mwaka kati ya wale wenye umri wa miaka 15-24 ikilinganishwa na wanaume (4690)

Wanawake na wasichana nchini Tanzania wanaendelea kubeba mzigo wa maambukizi ya VVU, hasa kutokana na kutokua na usawa wa kijinsia, kijamii na kiuchumi (Tamko la UNAIDS 2019). Moja ya sababu kubwa ya wanawake na wasichana kuendelea kulemewa na maambukizi ya VVU ni pamoja na unyanyasaji wa majumbani na mimba za utotoni. Imeripotiwa kwamba wanawake wanaopitia ukatili kutoka kwa wenzi wao wanauwezekano mara 1.5 zaidi kupata maambukizi ya VVU kuliko wanawake ambao hawapitii ukatili wa kijinsia.

#### **b) Athari za kiafya za ndoa na mimba za utotoni**

Kwa mujibu TDHS uzazi kwa wasichana balehe 1000 wenye umri wa miaka 15-19 uliongezeka kutoka 116 hadi 132 kati ya 2010 na 2015/2016. Hii ni moja ya viwango vya juu zaidi duniani. Familia nyingi huoza watoto wao kwa faida ya





kupata ng'ombe na gharama nyingine za kifedha. Ndoa za utotoni zinamadhara mengi ya kiafya kwa wasichana, familia, jamii pamoja na taifa.

- Mimba nyingi za utotoni hutokea katika maeneo ya vijijini (ambapo mwaka 2015/16, asilimia 31 ya wasichana wadogo walikuwa wajawazito au walikuwa na mtoto
- Mimba na ndoa za utotoni huongeza ukosefu wa usawa wa kijinsia na ukosefu wa elimu kwa wanawake na wasichana. Ukosefu wa elimu kwa wasichana unaweza kusababisha ukosefu wa fedha za kutosha kwa wanawake, kitu ambacho huchochea wanawake na wasichana kujihusisha na tabia hatarishi kama vile ukahaba, unywaji pombe na matumizi ya madawa ya kulevya ambayo ni hatari kwa afya.
- Takwimu zinaonesha kwamba wasichana wanaolewa mapema wanapata watoto mapema zaidi na wana uwezekano wa kupata watoto wengi zaidi. Hii husababisha ongezeko la idadi ya watu kwenye familia hivyo kushindwa kukidhi mahitaji muhimu kama lishe bora kwa watoto na wanawake.
- Ongezeko la idadi ya watu katika familia pia unaweza kusababisha upungufu wa fedha, ambayo inaweza kutumika kulipia huduma za afya kwa wanafamilia na hasa watoto.
- Pia, ukuaji wa haraka wa idadi ya watu unaweza kuwa na athari katika bajeti za afya za serikali ili kufidia gharama za afya.

### c) Vifo vya akina mama na vifo vya watoto

Kwa mujibu wa utafiti wa Shirika la Afya Duniana (WHO) kuhusu afya ya wanawake na ukatili majumbani ulibaini kuwa asilimia 7 ya wanawake walipigwa na wapenzi wao wakati wa ujauzito. Jijini Dar es Salaam, asilimia 38 ya wale waliopigwa wakati wa ujawazito waliripoti kupigwa ngumi au kupigwa kwenye sehemu ya tumbo, wakati Mbeya ikiwa asilimia 12 na asilimia 23. Ukatili majumbani unahusishwa na changamoto nyingi za uzazi ukiwemo vifo vya kinamama au madhara ya baadaye kwa mtoto mchanga. Takwimu za shirika la Afya Duniani zinaonyesha kwamba;

- Ukatili majumbani ni hatari na unaweza kuleta madhara kwa mama mjamzito na mtoto wake ambaye hajazaliwa. Athari hizo ni pamoja na mtoto kuzaliwa na uzito mdogo, kuharibika kwa mimba au kupata uchungu wa mapema zaidi, kuumia sehemu za mwili, kuwa na wasiwasi pamoja na matatizo mengine ya akili kwa mama wakati wa ujauzito ambayo yanaweza kuathiri afya ya akili ya mtoto baadaye katika maisha yake.



- Watoto waliozaliwa na mama ambaye alipitia vipigo wakati wa ujauzito wana uwezekano mkubwa wa kupata lishe duni wakati wa utoto wao.
- Wanawake ambao wanapitia ukatili wakati wa ujauzito wanaweza kupata matatizo ya kiafya ambayo huongeza idadi ya vifo vinavyotokana na ujauzito.
- Takwimu za hospitali nchini Tanzania zinaonyesha kuwa mimba za utotoni zinachangia kwa kiasi kikubwa vifo vya akina mama wajawazito. Inakadiriwa kuwa wasichana walio chini ya umri wa miaka ishirini wanachangia takribani asilimia 20 ya vifo vya akina mama, wakati kundi hilo lenye umri wa miaka 15 - 24 linachangia hadi asilimia 40 ya vifo vyote vya akina mama nchini. Ripoti hiyo inaonyesha kuwa kina mama vijana na wasichana walioolewa katika umri mdogo wako katika hatari zaidi ya kukumbwa na ukatili majumbani. (Girls Not Bride, 2018)

Tarehe 23 Aprili, 2021 wakati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipohutubia Bunge, alisema Serikali imedhamiria na kuweka kipaumbele katika kupunguza vifo vya akina mama wajawazito. Hata hivyo, Kutunga sheria dhidi ya ukatili majumbani kunaweza kuchangia kupunguza vifo kwa akina mama wajawazito.

Ukatili majumbani pia unaongeza uwezekano wa vifo vya watoto nchini ya umri wa miaka 5; kwa mfano, wanawake wengi, hasa katika maeneo ya vijijini, hawana maamuzi juu ya lini na jinsi ya kupata watoto na kwa muda gani wa kupata watoto. Wakati na jinsi ya kupata watoto hufanywa hasa na wanaume na shinikizo kutoka kwa familia. Kulingana na takwimu za TDHS, watoto wanaozaliwa ndani ya muda mfupi wanachangia ongezeko la vifo vya uzazi. Kwa mfano, kiwango cha vifo vya watoto wa chini ya miaka 5 ambao wamekishana na waliowatangulia chini ya miaka miwili huchangia mara mbili zaidi ya vifo vya watoto kuliko wale waliozaliwa baada ya miaka miwili.

#### **d) Majeraha ya mwili**

Ukatili majumbani husababisha majeraha ya kimwili ambayo huhatarisha afya ya mhanga. Inakadiriwa kuwa takribani nusu ya wanawake walio pitia mazingira ya ukatili majumbani Tanzania wanajeruhiwa kimwili na wapenzi wao na kwamba wengi wao wanauguza majeraha mbalimbali.

- Shirika la Afya Duniani (WHO) linakadiriwa kuwa takribani asilimia 40 ya wahanga wote wa ukatili majumbani nchini Tanzania wamejeruhiwa. Majeraha ambayohayaja sababisha vifo kama kichwa, shingo, au uso, ikifuatiwa na majeraha ya mifupa na sehemu za siri.



- TDHS inaripoti kuwa, kwa ujumla, asilimia 70 ya wanawake ambao wamewahi kupitia ukatili wa kimwili au kingono wamepata aina moja au zaidi ya majeraha. Aina ya kawaida ya majeraha ambayo waathirika wengi wamepata ni michubuko, kukatwa na kuunguzwa. Baadhi yao wamepata maumivu ya kichwa, mgongo, mifupa iliyovunjika, matatizo ya ujauzito, pamoja na magonjwa ya zinaa (STDs) na matatizo ya tumbo.

#### e) Majeraha mabaya (Mauaji ya Wenza)

Taarifa za vyombo vya habari hivi karibuni vimeonyesha ongezeko la mauaji ya wanawake yaliyofanywa na wenzi wao, kwa sababu ya wivu wa mapenzi. Ikumbukwe kwamba ripoti hizo pia huonesha kwamba hata wanaume ni waathirika wa aina hii ya ukatili japo sio kwa kiwango kikubwa kama wanawake na Watoto. Mwaka 2019, kupitia ufwatiliaji wa vyombo vya habari, uliofanywa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu matukio 12 ya mauaji ya wanawake yaliripotiwa, na 8 kati yao yalichangiwa na wivu wa mapenzi. Mwaka 2020, kupitia ufwatiliaji wa haki za binadamu na uchunguzi wa vyombo vya habari, uliofanywa na kituo hicho hicho kilibaini matukio 32 ya mauaji ya wanawake kutoka kwa wenzi wao yaliyorekodiwa, ambapo 23 yalichochea na wivu wa mapenzi.

Mwaka 2015 Shirika la Kimataifa la Amnesty liliripoti kuwa wanawake 26 katika mji wa Mbeya na 27 mkoani Geita waliuawa kutokana na ukatili majumbani. Hata hivyo, hakuna taarifa rasmi au zilichchapishwa na chanzo huru juu ya idadi halisi ya wanawake au wanaume waliouawa na weza wao, lakini mauaji yanayotokana na ukatili wa ndani yanaonekana kuongezeka nchini Tanzania

#### f) Gharama za afya kwa Taifa

- Ushahidi unaonyesha kuwa Serikali inaweza kupata gharama ya shilingi bilioni 27,391,620,000/Tsh kwa miaka 5 katika kukabiliana na ukatili wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na ukatili majumbani. Hii ni kwa mujibu wa bajeti ya MTAKUWWA 2016/2017-2021/22 katika eneo la utoaji huduma kwa wahanga wa ukatili.
- Wanawake na watoto wanaojeruhiwa wakati wa ukatili majumbani, wanapokea aina fulani ya huduma za matibabu, kama vile huduma za gari la wagonjwa, vipimo na matibabu, huduma za ushauri wa kisaikologia au tiba ya kimwili katika hospitali za serikali. Swala hili huongeza uhitaji kwa serikali kutenga bajeti zaidi katika kuboresha miundombinu ya upatikanaji wa huduma za afya.



## MAPENDEKEZO

Serikali imeonyesha nia ya kukomesha ukatili dhidi ya wanawake na watoto, ikiwa ni pamoja na ukatili. Pamoja na jitihada hizo, Serikali inapaswa kufanya yafuatayo ili kutokomeza ukatili majumbani nchini Tanzania.

1. Serikali inapaswa kutunga Sheria dhidi ya unyanyasaji wa majumbani. Kampeni, utoaji elimu na uhamasishaji hazitatosha kumaliza ukatili majumbani bila kutunga sheria na kuhakikisha utekelezaji wa sheria hiyo ili kuzuia ukatili majumbani. Kuwepo kwa kisheria pamoja na utekelezaji wake kunaweza kuchochea jamii kubadili mitazamo yao juu ukatili dhidi ya wanawake.
2. Serikali iwekeze hasa katika kuimarisha mifumo ya huduma za afya kwa wahanga wa ukatili hasa ukatili wa Majumbani. Kwa mfano, kuongeza idadi ya Vituo vya mkono kwa mkono (OSC) na nyumba salama.
3. Madawati ya Jinsia na watoto katika vituo vya polisi yanahitaji kujengewa uwezo na kupunguza vikwazo vya upatikanaji wa huduma, kama vile fomu ya polisi namba 3 (PF3). Fomu hizi zinapaswa kupatikana katika vituo vya afya ili kuepuka ucheleweshwaji wa huduma kwa wahanga.
4. Kushirikisha viongozi wa jamii, na viongozi wa dini kama sehemu muhimu ya kuwezesha mabadiliko ya kijamii na kitamaduni dhidi ya ukatili majumbani. Viongozi wa dini wanapaswa kuwezesha ili kushawishi jamii zao juu ya athari za ukatili majumbani na kuwasaidia kuwa watetezi wa haki za wanawake na watoto.

Utafiti zaidi unahitajika ili kupata takwimu halisi juu ya madhara ya kiafya yatokanayo na ukatili majumbani.

### **Kuhusu Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF)**

Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika, ni mtandao wa mashirika ya watu binafsi katika Bara la Afrika ambao unafanya kazi za kupinga haki za wanawake, kujitolea kukuza na kuimarisha mikakati inayounganisha sheria na maendeleo ili kuongeza ushriki wa ushawishi wa wanawake katika mikakati na pia kueneza chachu hiyo katika ngazi ya jamii, kitaifa na kimataifa.

WiLDAF ilisajiliwa nchini Tanzania mnamo mwaka 1997 chini ya Sheria ya Makampuni Sura ya 212 kama Shirika lisilo la kiserikali, lisilo la kisiasa na lisilojiendesha kwa faida.



WiLDAF Tanzania ina njozi ya kuona jamii ya Tanzania inayoheshimu haki za binadamu za wanawake. Misheni ni kujenga ni kujenga mtandao imara kwa ajili ya kukuza heshima kwa haki za binadamu za wanawake kupitia utetezi, usambazaji na uangalizi wa vyombo mbalimbali vya kitaifa na kimataifa pamoja na mpango wa dharura wa kuitikia ukatili wa kijinsia katika ngazi zote wakati huo huo ikihusisha sheria na maendeleo.

### **Kuhusu Mradi wa Uchechemuzi kwa Kutumia Takwimu (DDA)**

Mradi wa uchechemuzi kwa kutumia Takwimu (DDA) ni mradi unaofadhiliwa na Shirika la Kimataifa liitwalo Freedom House pamoja na PACT Tanzania.

Mradi huu ambao ni wa miaka mitano unakusudia pamoja na mambo mengine kutumia takwimu kama sehemu ya kushawishi mabadiliko ya Sera na Sheria ambazo zinalinda na kutetea haki za binadamu.

Mradi huu unafanya kazi kwa kupitia vikosi kazi (WGs) mbalimbali. WiLDAF inaratibu kikosikazi namba mbili (WG2) ambacho kimejikita katika kusimamia haki za Wanawake, Watoto, Vijana na watu wenye ulemavu.

## **SHUKRANI**

Taarifa hii fupi ni mchango wa watu binafsi, mashirika na wanachama wa kikosi kazi namba 2 ambao kwa pamoja wameshiriki katika kuandaa taarifa hii.

Kwa niaba ya kikosi kazi namba 2 (WG2), WiLDAF inapenda kutambua juhudi iliyofanywa na muandishi Iddi Rajabu Mziray kwa kujitolea kwake katika kuandaa rasimu ya awaliya taarifa hii fupi.

Vile vile tunatoa shukrani kwa Mkurugenzi wa WiLDAF Anna Kulaya kwa kuhariri taarifa hii fupi.

WiLDAF inapenda kuwashukuru wafuatao kwa kupitia na kuchangia katika kuboresha taarifa hii fupi; Bi Zakia Msangi, Bi Miriam Azaria, Asajile Mwakyusa, Simoni Songeraeli, Michael Lwakatare pamoja na Bi Annet Mushi.

Mwisho, shukrani ziende kwa wanachama wa WG2 ambao wameshiriki kikamilifu katika kuandaa taarifa hii fupi kama ifuatavyo;

1. Women in Law and Development in Africa (WiLDAF),
2. Tanzania Child Right Forum (TCRF),



3. Tanzania Domestic Workers Coalition (TDWC),
4. Mwanza Children and Youth Network (MCYN),
5. Tanzania Early Childhood Development Network (TECDEN),
6. Zanzibar Female Lawyers Association (ZAFELA),
7. Tanzania Association for children Advancement (ZACA),
8. Women Legal Aid Centre (WLAC),
9. Women with Disability Network (SHIVYAWATA),
10. Youth Partnership countrywide (YPC),
11. Gender and Adolescence Initiative (GAI)
12. Vijana Pambana Pata Maendeleo Rukwa (VIPAMARU),
13. Jitambue Lembuka,
14. Health Integrated Multispectral Services (HIMS),
15. Women Development for Science and Technology Association (WODSTA).

## MAREJEO

1. Tanzania (2015-16); Utafiti wa Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya Tanzania (TDHS) 2015-16.
2. Shirika la Kimataifa la Amnesty (AI). 25 Februari 2015. 'Tanzania.' Ripoti ya Kimataifa ya Shirika la Kimataifa la Amnesty 2014/15: Hali ya Haki za Binadamu Duniani. [Imepitiwa 24 Julai 2021].
3. Tanzania Bara (2020); Tathmini ya Jinsia ya Mwitikio wa Kitaifa wa VVU/ UKIMWI, 2020.
4. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (2020); Ripoti ya Haki za Binadamu Tanzania, 2020.
5. Shirika la Afya Duniani (WHO) (2005): Utafiti kuhusu Afya na Unyanyasaji wa Majumbani dhidi ya Wanawake, 2005 Tanzania Mainland (2020);
6. Tathmini ya Jinsia ya Mwitikio wa Kitaifa wa VVU/ UKIMWI, Muhtasari wa Sera, 2020.
7. Shirika la Afya Duniani; Makadirio ya kimataifa na kikanda ya unyanyasaji dhidi ya wanawake: kuenea na athari za afya juu ya unyanyasaji wa wapenzi wa karibu na unyanyasaji wa kijinsia usio wa mapenzi, 2010
8. Reuters. 25 Julai 2013. Kizito Make. "Ukatili wa Kijinsia Nchini Tanzania." [imepitiwa 3 Julai 2021]
9. ICRC, 2018: "Athari za kiuchumi za ndoa za utotoni: matokeo muhimu Julai 2018).
10. Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP). 2001. Ripoti ya Ufuatiliaji wa VVU / UKIMWI / STI Nambari 16. Dar es Salaam: Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, Wizara ya Afya.





## **Imechapishwa na WiLDAF, 2021**

Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo barani Afrika  
Eneo la Mikocheni A. Mtaa wa WiLDAF, Block F. Ploti Na. 635.  
S.L.P 76215, Dar es salaam, Tanzania

**Simu:** +255222701995,

**Barua pepe:** [wildaftanzania@gmail.com](mailto:wildaftanzania@gmail.com) / [info@wildaftanzania.or.tz](mailto:info@wildaftanzania.or.tz)

**Tovuti:** [www.wildaftanzania.or](http://www.wildaftanzania.or)